JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO

**BODI YA KAHAWA TANZANIA**

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Ref Na: CA.23/220/01/19** **23 Julai, 2024**

KWENDA : Viwanda Vyote Vya Ukoboaji Kahawa

: Wauzaji wote wa Kahawa Kwa njia ya Soko la Moja kwa Moja.

YAH: **KUWASILISHA SAMPULI ZA KAHAWA INAYOUZWA KWENYE SOKO LA MOJA KWA MOJA (DE) ILI KUPATIWA CHETI CHA UBORA**

Rejea kichwa cha habari hapo juu

2. Bodi ya Kahawa inawakumbusha wauzaji wa kahawa kwenye soko la moja kwa moja kuhakikisha kuwa wanapoomba kibali cha kuuzaji wa kahawa kwenye soko hilo watume 1kg ya sampuli ili kahawa hiyo ifanyiwe mchanganuo (Analysis) ili kubaini muonjo wa kahawa hiyo ili kupatiwa cheti cha ubora na kufanya tathmini ya kubaini iwapo bei iliyotolewa kwenye mkataba ipo juu ya kahawa yenye ubora huo kwa wastani wa minada mitatu/soko la dunia kama inavyohitajika kwenye kanuni zinazosimamia zao la kahawa (Coffee Industry Regulations 2023)

2. Bodi kama mtatuzi/msuluhishi wa hatua za awali za migogoro kwenye tasnia ya kahawa huweka kiasi cha sampuli hizi kama rejea (Reference Sample) iwapo kutatokea mabishano kwenye ubora wa kahawa. Viwanda vyote pia mnakumbushwa kutunza 300g ya sampuli kwenye maabara zenu ili zitumike kwenye utatuzi wa migogoro iwapo itatokea.

3. Hivyo ili maombi ya mauzo ya kahawa kwa njia ya moja kwa moja yafanyiwe kazi kwa haraka ni vema kabla hujapakia (Upload) mkataba utume sampuli za kahawa hiyo Bodi ya kahawa.

4. Tunawatakia utekelezaji mwema

F. J. Nyarusi

Kny; **MKURUGENZI MKUU**

KAHAWA HOUSE, 09 BR. J.K.NYERERE; S. L. P. 732, 25101 MAWENZI, MOSHI; Simu: 255 27 27 52324

**Barua Pepe:** info@coffee.go.tz; **Tovuti:** www.coffee.go.tz